

Uhalisia wa Utumwa wa Mwanamke katika Karne ya 21: Mfano wa Tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*

*Lina Akaka*¹

Ikisiri

Tatizo la utumwa hufikiriwa kuwa ni la zamani, wakati ambapo Waafrika waliuzwa kama bidhaa ili wakatamike katika mataifa ya Marekani Kaskazini na visiwa vya Karibiani. Utumwa ungalipo. Ingawa utumwa kama ule haupo kwa sasa, sura zake zinajichomoza kwa namna mbalimbali. Ingawa utumwa, uliokuwapo katika karne ya 18 na 19 hauko hai, umechukua mkondo mpya. Hivi leo wanawake wa Kiafrika huenda katika nchi za Mashariki ya Kati na Eneo la Ghuba kwa hiari yao tofauti na wanawake waliopelekwa kwa nguvu. Hata hivyo, wote hatima yao ni moja wote huishia kuwa watumwa. Hali hii na nyinginezo za kiutumwa zimewavutia wanafasihi kutumia jukwaa la fasihi kuakisi suala hili katika kazi zao. Mtafiti aliiteua kimakusudi tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* iliyoandikwa na Wa Mberia (2025) ili kuchunguza namna mwanamke wa anavyotumikishwa katika karne ya 21. Mkabala wa Bales (2012) wa haki za binadamu na utandawazi uliongoza utafiti huu. Makala inatumia tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* kuchunguza tajiriba za mwanamke katika utumwa pamoja na madhila yake katika karne ya 21, hususani katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Makala hii, pamoja na mambo mengine, inaonesha kuwa utumwa bado unaendelea na wanawake, kwa kiasi kikubwa, wamekuwa wahanga wa mfumo huu dhalimu.

1.1 Utangulizi

Licha ya kuwa hatua kubwa zimepigwa katika diskosi za haki za wanawake ulimwenguni, karne ya 21 inazidi kufichua aina tofauti za utumwa wa wanawake zinazoendelezwa. Baadhi ya utumwa huo ni ukandamizaji wa wanawake, ubidhaishaji na utumwa ulioratibiwa ambao umefichika katika taasisi za sasa, kaida za kitamaduni na mifumo nguvu ya kibabedume. Wasomi wanakubaliana kuwa utumwa wa sasa wa wanawake hauwafungi kwenye minyororo bali unadhihirika kupitia utegemezi wa kiuchumi, kukosa sauti, unyonyaji wa kingono, udhibiti wa kinyumbani na mashambulizi ya kijinsia ambayo hupunguza uhuru wa mwanamke

¹ Mhadhiri, Idara ya Lugha na Sanaa za Maonesho, Chuo Kikuu cha Daystar, Kenya
Baruapepe: lakaka@daystar.ac.ke

(Institut Genre en Geopolitique-IGG-GEO, 2020; Free, 2023). Kwa hivyo, utumwa wa sasa wa wanawake ni uhalisia wa jamii ingawa unatofautiana kutoka jamii moja hadi nyingine kutegemea muktadha, utamaduni, mifumo ya imani na taasisi za kibabedume (Bales, 2016).

Utumwa wa karne ya 21 si wa kufungwa kwa minyororo na kuuzwa sokoni kama bidhaa. Utumwa wa enzi hizi umebadilika, si dhahiri. Hata hivyo, utumwa wa enzi hizi bado ni wa kikatili kama ulivyokuwa wa zamani. Wanawake ulimwenguni kote huteseka kutokana na utumwa wa kisasa ambao hujumuisha kazi za kulazimishwa, utumishi wa nyumbani na unyonyaji kwa misingi ya jinsia. Licha ya kuwa kuna sheria za kimataifa na mikataba ya haki za binadamu inayolinda binadamu dhidi ya dhuluma, mataifa ya Mashariki ya Kati yangali yanakiuka haki za binadamu kwa kiwango kikubwa. Dhuluma hizi zinachochewa na umaskini, kutokuwapo kwa usawa wa kijinsia, ulinzi hafifu wa kisheria na ubidhaishaji wa miili ya binadamu (Rami na wenzake, 2025).

Inakadiriwa kuwa asilimia 70 ya watu milioni 40.3 ambao wako katika utumwa wa kisasa ni wanawake na wasichana, (Boyle na Shields, 2018). Hii ni kinyume na hali ilivyokuwa katika karne ya 18 ambapo wanahistoria wanakadiriwa kuwa kati ya asilimia 65-70 ya Waafrika waliosafirishwa kupitia bahari Atlantiki walikuwa wanaume na wavulana (Lovejoy, 2011). Uhitaji mkuu wa wafanyakazi wa kiume ulivutiwa na kazi za kulima katika mashamba makubwa, migodi na ujenzi ambapo nguvu zilihitajika. Campbell (2004) anadai wakati huohuo, wanawake wengi walisafirishwa kupitia bahari ya Hindi wakipelekwa katika mataifa ya Mashariki ya Kati ambapo utumishi wa kazi za nyumbani ulihitajika. Wakati huo walimilikiwa kisheria na bwana wa watumwa kinyume na utumwa wa enzi hizi ambao unaendelezwa kinyume cha sheria. Utumwa mpya wa karne ya 21 huwaweka watu chini ya udhibiti mkali wa kulazimishwa bila kudai umiliki wao wala kuwajibika kwa maisha yao (Bale, 1999).

Kwa mujibu wa Morgan (2004), wanawake waliokuwa chini ya utumwa walitumikishwa wakati wa shughuli za uzazi na mashambani pia. Mabwana waliiona miili ya wanawake kama rasilimali za kiuchumi, hivyo, uwezo wa mwanamke wa uzazi ukawa jukumu la kiuchumi la utumwa. Hali hii inajitokeza pia katika utumwa wa enzi hizi ambapo Daghar (2020) anadai asilimia 19 ya wanawake wanaokwenda katika mataifa ya Mashariki ya Kati hunyanyaswa kingono.

Hata hivyo, hatimaye biashara ya watumwa ya Kiatlantiki ilipigwa marufuku na Uingereza katika mwaka wa 1807 kupitia sheria ya biashara ya utumwa ambayo iliharamisha ununuzi na uuzaji wa watumwa katika dola ya Uingereza (Davis, 1985). Davis anadai upigaji marufuku huo ulichochea na mabadiliko ya kimawazo na kimaadili ya Uingereza na himaya nyingine zikafuata mkondo huo. Lovejoy (1983) anadai kuwa, ingawa mataifa ya Ulaya yalizipiga biashara za watumwa marufuku mapema katika karne ya 19, biashara hiyo imechukua sura mpya katika mataifa ya Mashariki ya Kati na Eneo la Ghuba.

Utumwa unaoendelezwa katika karne hii unachunguzwa na wanataaluma mbalimbali wakiwamo wanasosholojia, wanaanthropolojia, wanasheria, wanahabari na wengineo. Suala hili limeanza kuwavutia pia wasanii wa kazi za fasihi kutumia kazi zao kuliangazia kwa sababu utumwa hukiuka haki za binadamu. Fasihi kama kioo cha jamii kinachoangaza masuala yanayomhusu binadamu haina budi kutumiwa na waandishi kupinga utumwa wa wanawake na kufichua uovu uliomo. Sinha (2021) anajadili jinsi wanawake kutoka mataifa ya Afrika na Asia wanavyofanya kazi katika mazingira magumu ya utumwa katika mataifa ya Mashariki ya Kati na eneo la Ghuba. Sinha anaeleza jinsi wafanyakazi wahamiaji wanavyotendewa katika mataifa hayo ni aina ya utumwa wa kisasa. Anaongeza kuwa utumwa umefanywa kuwa jambo la kawaida, likataasisishwa na kuenea kwa kiwango kikubwa katika mataifa hayo.

Fasihi inaendelea kutumika kama kioo cha kufichua, kudadisi na kuhakiki mifumo iliyofichika ya utumwa ambayo ingali inamkandamiza mwanamke katika karne ya 21. Tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* ni matini ya kisanaa yenye nguvu inayoigiza aina tofauti za ukandamizaji wa kisaikolojia na kitamaduni ambao umekitwa katika jamii za kibabedume. Kupitia kwa wahusika, migogoro na ukuzaji wa maudhui, tamthilia inaangazia utumwa wa mwanamke, kukosa sauti kwake na uhalalishaji wa kaida zinazomfunga mwanamke licha ya utetezi wa wanawake ulimwenguni.

Kwa hivyo, tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* ni matini muhimu ya kurejelea kuhusiana na masuala ya utumwa wa wanawake na kudadisi jinsi fasihi ya sasa inavyoakisi minyororo isiyoonekana ambayo ingali imewafunga wanawake leo. Makala hii inachunguza uhalisia wa utumwa wa wanawake katika karne ya 21 kwa kurejelea tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*. Uchanganuzi huu unaonesha namna matini inavyofichua ukandamizaji, unyonyaji, ubaguzi na dhuluma za kingono wanazokabiliana nazo wanawake katika ajira.. Pia, unaonesha jinsi fasihi kama hii inavyotoa mchango kwenye mijadala kuhusu haki za jinsia, uhakiki wa masuala ya kifeministi na uhuru katika jamii za Kiafrika.

1.2 Tafiti kuhusu Wanawake, Utumwa na Fasihi

Suala la utumwa wa sasa limevutia mitazamo tofauti ya kitaaluma katika tafiti. Baadhi ya taaluma hizo ni sosholojia, sheria, anthropolojia, uchumi, saikolojia, taaluma ya habari, siasa na mahusiano ya kimataifa, teknolojia na data ya sayansi, na jinsia na masuala ya kike. Suala hili limeanza kuwavutia pia waandishi wa kazi za fasihi kutumia kazi zao kuliangazia kwa sababu utumwa hukiuka haki za binadamu. Fasihi kama kioo cha jamii kinachoangaza masuala yanayomhusu binadamu haina budi kutumiwa na waandishi kupinga utumwa wa wanawake na kufichua uovu uliomo. Sinha (2021) anajadili namna wanawake kutoka mataifa ya Afrika na bara la Asia wanavyofanya kazi katika mazingira magumu na hali ya utumwa katika mataifa ya Mashariki ya Kati na Eneo la Ghuba.

Drescher (2009) anadai kwamba biashara za watumwa zilitambuliwa rasmi kisheria ndani ya himaya ya Ulaya kuanzia karne ya 15 na kuwa shughuli muhimu katika uchumi wa kikoloni wa Atlantiki. Drescher anaendelea kueleza kuwa mamilioni ya Waafrika walinaswa, waliuzwa na kusafirishwa hadi katika mashamba makubwa huko Marekani Kaskazini na visiwa vya Karibiani. Waafrika waliouzwa walimilikiwa kama mali ya mtu binafsi; walinunuliwa, waliuzwa au kurithiwa. Utumwa ulihusishwa na masuala ya rangi. Waafrika na vizazi vyao walionekana kuwa duni na waliwekwa utumwani kwa misingi ya rangi.

Sinha (2021) alichunguza jinsi wafanyakazi wahamiaji wanavyotendewa katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Aligundua kuwa wanawake wengi ndio walitumika nyumbani huku mazingira ya kazi yakiwa mabaya sana. Walifanya kazi kwa muda mrefu bila kupumzika na wakati mwingine hawakupewa muda wa kulala. Halikadhalika, walinyimwa chakula, walinyanyaswa kingono na kubaguliwa kwa misingi ya rangi. Makala ya Sinha inaeleza jinsi wafanyakazi wa kike wanavyotumikishwa katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Inajadili dhuluma za kitaasisi pamoja na mfumo wa *kafala* unaoendeleza utumwa wa kikatili. Chini ya mfumo wa *kafala*; viza, makao na hadhi ya kisheria ya mfanyakazi hutegemea mwajiri aliyemdhamini. Kwa hivyo mfanyakazi hawezi kubadilisha kazi, kuondoka nchini au hata kuacha kazi bila kuruhusiwa na mwajiri wake.

Mann (2010) alichunguza ulanguzi wa binadamu kutoka mabara ya Asia na Afrika hadi mataifa ya Mashariki ya Kati. Mann anadai Mashariki ya Kati ni eneo linalounganisha Asia, Afrika na Ulaya na kutumika kwa ulanguzi wa watu kutoka katika mataifa maskini hadi mataifa tajiri. Watu hao wanapohamishwa kutoka mataifa yao hususani kwa udanganyifu, huishia katika utumwa wa kingono, ombaomba na ujakazi wa nyumbani.

Shureteh, Al-Khalili na Neimneh (2021) walichunguza riwaya ya *Slaves' Peanuts* (2016) iliyoandikwa na Khrais ambapo ameuonesha utumwa kama njia panda katika karne ya 20. Riwaya hiyo inatoa taswira ya utumwa wa wanawake katika enzi zisizo za utumwa. Suala hilo linavunja moyo na kuibua hisia za kumbukumbu jinsi Wareno walivyohusika katika biashara za watumwa katika kipindi cha ukoloni na athari zake kwa watu wa sasa wa ulimwengu wa tatu.

Mutembei (2016) alichunguza utumwa na nafasi yake katika fasihi ya Kiswahili. Anadai kuwa utumwa umeacha athari kubwa ya kijamii na kisaikolojia kwenye jamii za Waswahili. Athari hizo zimevuka mipaka hadi kwenye taasisi za kihistoria na kuathiri kumbukumbu za kitamaduni na tafakuri za kifasihi. Akitumia nadharia ya Mwingiliano Matini, Mutembei anaeleza namna kumbukumbu za utumwa zinavyoundwa na kuundwa upya katika matini za Kiswahili kama vile *Uhuru wa Watumwa* (1934), *Maisha ya Tippu Tip* (1966) na *Tendehogo* (1984). Mutembei (2016) anadai kazi hizi hazifichui tu ufungwa waliopitia watumwa bali utumwa wa kiakili pia ulioendelezwa kwa miaka mingi baada ya utumwa kupigwa marufuku. Isitoshe, Mutembei anaangazia kuzuka kwa upinzani na uzinduzi katika kazi za kifasihi huku akionesha namna waandishi wa Kiswahili wanavyoendelea

kushughulikia suala la utumwa kama tajiriba waliyopitia Waafrika na kama sitiari ya ukandamizaji wa kijamii na kisaikolojia.

Fasihi ya Kiswahili inaangazia aina nyingi za utumwa ukiwamo wa kikoloni mamboleo. Ikuathu (2017) akieleza maudhui ya ukoloni katika tamthilia za *Mstahiki Meyu* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2009) anaonesha jinsi mataifa huru ya Afrika Mashariki yalivyo chini ya utumwa wa kifedha. Utumwa huo, kwa mujibu wa Ikuathu (2017), unatekelezwa dhidi ya mataifa huru ya Afrika. Mashirika yanayoendeleza utumwa huo ni kama vile Benki ya Dunia, Shirika la Fedha Duniani na Shirika la Kibiashara la Dunia. Mataifa yanayoendelea yamekuwa katika utumwa wa kifedha kwa sababu ya mikopo mikubwa ambayo yanakopa na kukosa kuitumia kwa maendeleo ya nchi. Hali hii husababisha umaskini na mataifa hayo kuendelea kuwa chini ya utumwa wa kifedha.

Tafiti zilizopitiwa zinadhihirisha kuwa utumwa wa wanawake ni suala lililoanza katika kipindi cha biashara za watumwa za bahari Atlantiki. Suala hilo, kama linavyodhihirika katika tafiti zilizopitiwa, limechunguzwa na wanataaluma mbalimbali wakiwamo wanafasihi ambapo matini za fasihi zinazoakisi suala hilo zimehakikiwa. Tahakiki zilizofanywa zinabainisha kuwa utumwa bado upo na ndiyo sababu kazi za fasihi zinazidi kuuakisi kwa lengo la kufichua maovu yanayotokana na utumwa huo.

2.1 Misingi ya Nadharia

Makala hii iliongozwa na mkabala wa Bales (2012) wa haki za binadamu na utandawazi ambao unauona utumwa wa sasa kama zao la ukosefu wa usawa wa kiuchumi ulimwenguni na ukiukaji wa haki za msingi za binadamu. Ingawa mkabala wa Bales unatokana na mawazo ya Umarx Mamboleo ya unyonyaji, unavuka mipaka ya mapambano ya kitabaka na kuisitiza mikabala ya kimaadili na kisheria ya ukiukaji wa haki za binadamu katika mifumo ya ajira za sasa. Mkabala wa Bales (2012) unafaa katika uchunguzi wa unyonyaji wa wafanyakazi wa nyumbani ambao tajiriba zao zinaakisi maporomoko ya heshima ya binadamu katika uchumi wa kilimwengu. Mkabala wa Bales unatoa mwongozo wa kufasiri taswira za utumwa wa sasa na unyonyaji. Bales (2012) anaeleza kuwa utumwa haujatokomea ila umebadilika na kuchukua sura mpya inayoendelezwa na mifumo ya kiuchumi ya ulimwengu na uhitaji wa nguvu kazi ya bei nafuu. Kulingana na Bales, utumwa wa sasa una sifa za umiliki usio wa kisheria pamoja na udhibiti kupitia udanganyifu, ufungwa wa madeni, vitisho na vizuizi vya uhuru wa kusafiri. Anatanabahisha kuwa utandawazi umezidisha ubidhaishaji wa nguvu za binadamu na kufanya vikundi fulani hususani vya wafanyakazi wa nyumbani na wengineo wahamiaji kuwa kama watu wasiokuwa na thamani katika uchumi wa kimataifa. Bales ameeleza aina tofauti za unyonyaji, dhuluma na ukatili unaofanyiwa wafanyakazi hao. Hivyo, masuala yaliyojadiliwa katika makala hii yamekitwa katika mihimili hii.

2.2 Mbinu za Utafiti

Mbinu ya utafiti huu ni ya uchanganuzi matini. Utafiti ulifanywa mtandaoni na maktabani ambapo data ya upili ilikusanywa kwa kusoma vyanzo mbalimbali vyenye masuala yanayohusiana na utumwa. Kundi lengwa la utafiti lilikuwa tamthilia ya Kiswahili na sampuli ya utafiti ilikuwa tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia* iliyoteuliwa kimakusudi kwa misingi ya maudhui ya utumwa yaliyomo. Mtafiti alikusanya data lengwa kwa njia ya usomaji makinifu wa tamthilia teule na kuzinakili kwa kutumia kalamu na daftari. Hatimaye, mada ndogondogo zikaibuliwa kutokana na data hiyo. Mtafiti alifasiri data hizo na kuzichanganua kwa kunukuu madondoo na kujadili yaliyomo huku akirejelea maoni ya wanazuoni mbalimbali kuhusu masuala yaliyojadiliwa.

3.1 Tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia*

Jeneza kutoka Saurabia ni tamthilia iliyochapishwa mwaka wa 2025. Iliandikwa na Kithaka Wa Mberia. Hii ndiyo tamthilia ya kwanza ya Kiswahili kuangazia suala la utumwa wa wanawake katika karne ya 21 ndani ya mataifa ya Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali. Tamthilia inaangazia tajiriba za wanawake mikononi mwa waajiri katika taifa la Saurabia. Uandishi wa tamthilia hii ulichochea na taarifa nyingi za vifo vilivyotangazwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii. Vifo hivyo vilitokana na mateso ya kisaikolojia, unyanyasaji wa kingono, kupigwa, kunyimwa chakula, kukosa uhuru wa kutangamana na ukiukaji wa haki nyinginezo za binadamu. Baadhi ya wafanyakazi huishia kujitoa uhai na wengine kuuawa na waajiri wao.

3.2 Taswira ya Utumwa wa Karne ya 21 katika Fasihi ya Kiswahili

Idowu na wenzake (2021) wanafafanua utumwa wa karne ya 21 kuwa ni wenye sifa za kudhibiti bila umiliki, vitisho vya mashambulizi au hata mashambulizi yenyewe. Sifa nyingine ni kupoteza uhuru na haki ya jinsi mtu atakavyoendesha maisha yake na unyonyaji wa nguvu za mtu bila malipo kwa kazi aliyofanya au kwa malipo duni. Tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia* inaakisi hali ya mambo inavyokuwa kutoka katika mchakato wa usafirishaji wa waajiriwa wa kike, maisha yao kazini na maafa wanayokumbana nayo chini ya waajiri katili. Tamthilia inapiga mwangwi simulizi ambazo zimetolewa kwa mashirika mbalimbali ya utafiti yanayochunguza hali za kikazi za wanawake wanaofanya kazi katika mataifa hayo ya Uarabuni. Katika sehemu zifuatazo, makala hii imechanganua baadhi ya maudhui yanayoakisi sifa za utumwa wa karne ya 21.

3.2.1 Udanganyifu

Kulingana na TUKI (2019), udanganyifu ni vitendo vya kughilibu watu au kufanya jambo ambalo mtu anajua ni la uongo. Udanganyifu hutumika sana katika maandalizi ya safari za kwenda Uarabuni kwa lengo la ajira. Mawakala hutoa taarifa zisizo za ukweli kuhusu ajira hizo hadi wanawake wanapoenda huko na kukumbana

na hali zilizo kinyume na matarajio. Hali hiyo hushuhudiwa sana katika mataifa ya bara la Afrika ambapo mawakala hutumia udanganyifu kuwapeleka wanawake katika mataifa ya Mashariki ya Kati na Mashariki ya Mbali ili kutumika nyumbani. Vlieger (2011) anashadidia wazo hilo anaposema kuwa mawakala wa nchi asili na mawakala wenzao wa kieneo huwapa watu taarifa za udanganyifu au zinazopotosha kuhusu kazi hizo, mishahara, saa za kufanya kazi, siku za kupumzika hata nchi wanazoenda. Vlieger anaendelea kueleza kuwa mfanyakazi anaweza kuambiwa kuwa anapelekwa Dubai lakini akapelekwa Saudi Arabia au taifa jingine lolote la Ghuba. Mawakala ndio wanaowezesha utumwa kwa kutumia udanganyifu kama inavyoakisiwa katika tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia*. Mhusika Nambi alihadaiwa na wakala wake kuwa alikuwa akipelekwa Dubai na badala yake akajikuta yuko Saurabia. Mwandishi anaeleza, katika uwanja wa ndege, Nambi na Halima wanapofika kwenye chumba kimojawapo katika kituo cha kukusanyia wasichana wanaokuja kufanya kazi katika Ufalme wa Saurabia, Zakiya anawakaribisha kwa mazungumzo yafuatayo:

- ZAKIYA: Karibuni katika Ufalme wa Saurabia.
 NAMBI: [akishtuka] Ufalme wa Saurabia.
 ZAKIYA: Ndiyo; bila shaka. Kwani unadhani mko wapi?
 NAMBI: Niliambiwa nilikuwa naenda Dubai.
 ZAKIYA: Ni nani aliwaambieni ulikuwa unaenda Dubai?
 NAMBI: Wakala wangu.
 ZAKIYA: Hayo ya Dubai siyajui na sina hamu kuyajua. Uko katika Ufalme wa Saurabia kufanya kazi na wala siyo kucheza. Ya Dubai yatoe akilini; yatupe mbali [Kwa Halima]. Wewe ulijua uko wapi? (uk. 17)

Katika dondoo hilo, Nambi anashtuka anaposikia kuwa walikuwa Saurabia. Hili linadhihirisha udanganyifu unaogubika michakato ya maandalizi ya safari na masharti ya ajira pia. Vlieger (2011) anadai kuwa mikataba baina ya waajiri na waajiriwa pia huletwa ikiwa imeandikwa katika lugha za kigeni ambazo waajiriwa tarajiwa hawaielewi. Waajiriwa hutia sahihi mikataba hiyo bila kuelewa masharti yaliyomo. Jambo hilo linaelekea kuchangia pia katika dhuluma wanazopitia chini ya waajiri wao katika mataifa ya kigeni. Bales (1999) anatalia nguvu mawazo ya Vlieger anaposema watumwa wa sasa hawanaswi kwa kutumia nguvu kama vile ilivyokuwa zamani. Mbinu za udanganyifu katika mchakato wa uajiri hutumiwa na mawakala wanapowapa wafanyakazi taarifa zisizo sahihi kuhusu mikataba ya kazi.

Katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*, udanganyifu huo ulijitokeza bayana. Isitoshe dalili za mateso atakayopitia Nambi zinaanza kuibuka mapema katika uwanja wa ndege. Zakiya, mhudumu katika kituo cha kupokea wafanyakazi wa kigeni anapomkagua Nambi kwa macho anamtia wasiwasi. Isitoshe anakataa

kumuonesha mahali atakapoenda kujisaidia anaposhikwa na haja ndogo kama inavyodhihirika katika dondoo lifuatalo:

- NAMBI: [kwa Zakiya, baada ya kurudi akiwa amevaa vazi alilopewa na mikononi ameshikilia mavazi aliyokuwa amevaa awali] Naomba kujua mahali pa kwenda kujisaidia.
- ZAKIYA: Tulia kwanza. Itabidi ufunze kibofu chako au utumbo wako nidhamu.
- NAMBI: Samahani; nimekunywa maji mengi.
- ZAKIYA: Hiyo ni shauri yako. Sitakuruhusu kuharibu utaratibu wangu wa kazi.
- NAMBI: Lakini...
- ZAKIYA: Lo! Nimekwambia ufunze kibofu chako nidhamu na bado unaniambia umekunywa maji mengi. Hiyo ndiyo sababu ya kukitaka kibofu chako kiwe na nidhamu. Kingekuwa hakina maji mengi hakungekuwa na umuhimu wa kukifunza manufaa ya nidhamu (uk. 17).

Maneno ya Zakiya katika dondoo hilo yanamtia hofu Nambi. Majibu yake yanakuwa mafupi na Zakiya anamkatiza usemi kwa hasira. Tayari mazungumzo hayo yanaonesha kuwa Nambi hatakuwa salama. Isitoshe, kabla ya kisa hiki, Zakiya alikuwa tayari ashamkemea Nambi kwa ajili ya vazi alilokuwa amevaa. Alimpa vazi jingine akidai kuwa alilokuwa nalo lilikejeli imani na maadili (uk. 16). Jambo hili linaashiria udhibiti na ukosefu wa uhuru wa kibinafsi. Mara nyingi, wanawake wanaoenda kutumikishwa katika mataifa ya Mashariki ya Kati hushurutishwa kuvaa mavazi ya Kiislamu, huwa hawana uhuru wa kuvaa wapendavyo. Mawazo hayo yanaungwa mkono na Laiboni na Njiru (2019) ambao wanadai kuwa utafiti uliofanywa miongoni mwa wanawake waliorudi kutoka mataifa hayo unaonesha kuwa walihitajiwa kuvaa mavazi yaliyoakisi utamaduni wa mataifa hayo pamoja na aina ya kazi walizokuwa wakifanya. Bales (1999) anaona jambo hili kama utumwa wa kikandarasi ambapo wanawake wanatia saina kandarasi ambazo zinawageuza kuwa watumwa chini ya masharti na udhibiti mkali kiasi kwamba wanakosa uhuru.

3.2.2 Ubaguzi wa Rangi

Mkataba wa Kimataifa wa Kutokomeza Aina Zote za Ubaguzi wa Rangi (ICERD) ni mkataba mkuu wa kisheria unaolenga kupambana na ubaguzi wa rangi duniani. Ulipitishwa na Baraza Kuu la Umoja wa Mataifa mwaka 1965 na ukaanza kutumika mwaka wa 1969 (Mutua, 2001). Licha ya sheria hiyo inayodhibiti ubaguzi kwa misingi ya rangi ya ngozi, waajiri katika mataifa ya Mashariki ya Kati wangali wanaendeleza desturi hiyo, (Sinha 2021). Wanawake wanapofika katika mataifa ya Mashariki ya Kati kwa shughuli za kazi, hushtuka kwa sababu ya tofauti za kitamaduni wanazokumbana nazo pamoja na mambo mengi wanayotendewa. Bales

(2005) anadai mambo mengi wanayotendewa ni ukiukaji wa haki za binadamu. Hivyo, tunaona kuwa Nambi anapofika kwa Sharifa mkewe Anwar, mwajiri wake, hampi nafasi ya kupumzika. Hii inakuwa ishara kuwa uhuru wake utatatizwa. Kwanza bila kujali hisia za Nambi, Sharifa anamwambia mume wake katika dondoo lifuatalo kwamba amemvunja moyo kwa kumletea mfanyakazi Mwafrika:

SHARIFA: [*Uso ukionyesha kutoridhika*] Ilikuwaje?

Mbona umenivunja hivi?

ANWAR: Sioni nimekuvunja vipi.

SHARIFA: Tulikubaliana nini?

ANWAR: Nitafute mfanyakazi.

SHARIFA: Basi, ikawaje?

ANWAR: Nikatafuta mfanyakazi.

SHARIFA: Ukaona ni sawa kuniletea ngozi nyeusi?

ANWAR: Wakala wa kuleta wafanyakazi kutoka ng'ambo alishindwa kupata mfanyakazi mwingine isipokuwa Mwafrika... (uk. 22)

Sinha (2021) anasema mitazamo kama hiyo inatokana na kuufanya ubaguzi kwa misingi ya rangi liwe jambo la kawaida. Ukawaida huo hujitokeza katika burudani, taarifa za habari, mazungumzo ya kawaida na maudhui ya mitandao ya kijamii ambayo huzalisha imani kwamba wafanyakazi wa nyumbani ni viumbe duni. Mazungumzo baina ya Anwar na mkewe katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* yanaibua taswira ya ubaguzi kwa misingi ya rangi ya ngozi. Anwar alisema kuwa hangeweza kupata wafanyakazi kutoka Bangladeshi, Thailand au Ufilipino (ambao huwa na ngozi nyeupe) kwa kuwa ingewabidi wasubiri kwa muda wa miezi miwili (uk. 22) na ndiyo kwa sababu akamleta mfanyakazi Mwafrika.

3.2.3 Ukandamizaji

Manzo (2005) anasema vipengele vya msingi vya utumwa wa kisasa vimetambuliwa kwamba ni udhibiti bila umiliki, matumizi ya nguvu na kupoteza uhuru na haki. Wanawake kutoka Afrika wanaojiriwa kufanya kazi za nyumbani hawamilikiwi kwa njia yoyote. Mikataba huwa dhahiri kwamba baada ya miaka miwili, inaweza kuhuishwa kutegemea bidii iliyooneshwa kazini na mfanyakazi (Njiru na Laibon, 2019). Hata hivyo, idadi kubwa ya wanawake hukandamizwa kwa njia mbalimbali. Bales (2002) anaeleza kwamba tangu enzi za kale utumwa ulimaanisha kupoteza uhuru wa kuchagua pia mashambulizi yaliyotekelezwa na mwaajiri. Sifa hizi zinajitokeza katika utumwa wa sasa ambapo wanawake wanakandamizwa kwa njia tofautitofauti kama inavyodhihirika katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*.

Sharifa anampangia Nambi kazi nyingi (kur. 24-25). Anamwambia atakuwa akiwasaidia kazi jamaa zao pia. Maagizo anayopewa yanachora taswira ya utumwa, isitoshe toni anayotumia anapotoa maagizo hayo ni kali, yenye dharau na

inayoonesha kuwa hawapo katika tabaka moja. Anasisitiziwa mapema kuwa yeye ni kijakazi anapomwambia amtambue kama memsahib (uk. 25). Anamkumbusha kumtaja kwa neno hilo tena katika uk. 32 Nambi anapoonekana kusahau. Katika utafiti waliofanya nchini Kenya miongoni mwa wanawake waliokuwa wamerudi nchini kutoka katika mataifa hayo, Njiru na Laibon (2019) wanaeleza kuwa mazingira ya kazi yalikuwa mabaya. Wanawake wengi walidhalilishwa na kunyanyaswa huku wakitukanwa kwa sababu ya rangi ya ngozi yao na imani za kidini. Tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* inamulika taswira hiyo kama ifuatavyo:

SHARIFA: [*Baada ya kwenda palipo na sinia na kukikagua chakula. Kwa Nambi; sauti ya kelele*] Zuzu! Gulagula! Zumbukuku! Bwege! Dufu! Uliniambia kabla ya kuondoka msituni Afrika ulionyeshwa jinsi ya kupika. Unathubutu kutuletea matabwatabwa! Yachukue urudi nayo jikoni ukapike chakula. Baradhuli kabisa! [*Nambi anabeba sinia na kuondoka*]

WISAM: [*ambaye anaonekana amekerwa na lugha ya mamake kwa Nambi*] Mama, kwa nini unamtusi? (uk. 28)

Sharifa anamtukana Nambi bila kuonja chakula akajua uzuri au ubaya uliomo. Alianza kumtukana baada ya kukikagua tu. Hata kama hakupendezwa na mapishi yake, angemweleza kwa njia nzuri. Sharifa anaonesha chuki kubwa dhidi ya watu Waafrika kama inavyodhihirika katika mazungumzo kati yake na Wisam, mwanawe, (kur. 27-28). Sharifa haamini kuwa Mwafrika anaweza kufanya kitu vizuri. Kwa mfano, anapoambiwa kuwa mwalimu wa hisabati ni Mwafrika, anauliza iwapo ni mwalimu au dereva wa shule. Mtazamo huu dhidi ya Waafrika unaonekana pia katika namna anavyomtendea Nambi baada ya mapishi, haamini kuwa Nambi anaweza kupika chakula kizuri. Hivyo, anaanza kumtukana akimwambia kuwa amewapikia matabwatabwa. Licha ya matusi ya kila wakati, Nambi hapewi chakula cha kutosha, muda wa kulala ni mfupi na anakosewa heshima.

NAMBI: [*kwa hadhira*] Kuna maisha yanayoeleweka na yasiyoeleweka; hali ya kustahimilika na isiyostahimilika; mateso yanayovumilika na yasiyovumilika. Chakula kinachoweza kuitwa chakula sipati; usingizi wa kutosha kuondoa machovu silali; heshima anayostahili binadamu, kwangu ni ndoto ya mbali kama nyota angani. Nikijaribu kuuliza swali najipata kwenye chaka la kinamasi; chaka lenye pogoo kavu zinazoporomoka na kunigonga kichwani; chaka lenye ukungu unaoziba njia mtu asijue pa kukanyaga (uk.13).

Njiru na Laibon (2019) wanasema mijadala baina yao na wanawake waliorudi ilifichua kuwa walikuwa wakifanya kazi kwa muda mrefu wa kati ya saa 17-20 kila siku. Nambi anamwambia rafiki yake Halima jinsi alivyokuwa akifanyishwa kazi hata za jamaa wa mwajiri wake, anasema:

NAMBI: Nitakukumbuka kwa miaka mingi. Nitakukumbuka kwamba nilipoishi katika kinamasi cha dhuluma, nilikuwa na rafiki ambaye alinifaa. [Kimya] Nilikwambia nafanya kazi zaidi ya nyumba moja. Mara nyingine natolewa kama mkopo kwa jamaa za waajiri wangu. Mara, “Nenda kwa fulani ukamsaidie kazi”, mara nyingine, “Kesho saa tano usiku, utaenda kwa fulani ukasaidie kuosha vyombo baada ya kumalizika karamu!” Basi, juzi nilichukuliwa kutoka kwa waajiri kuenda kusaidia kazi baada ya karamu. Niliponea chupuchupu. Karibu nione kilichomtoa kanga manyoya! (uk. 68).

Nambi hakupewa hata siku moja ya mapumziko wala fidia kwa sababu ya kufanya kazi mfululizo bila kupumzika. Isitoshe, alinyimwa mshahara na jitihada zozote za kuudai zilizua matusi. Fasihi kama sanaa inayoakisi uhalisia wa maisha inaakisi hayo katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* katika mazungumzo yafuatayo kati ya Sharifa na Nambi:

NAMBI: Mambo. Miezi mitano baada ya kuondoka nyumbani kwenda ughaibuni kufanya kazi sijawatumia chochote ilhali niliwaacha katika shimo la uchochole. Niliwaahidi nitakuwa nikiwatumia pesa za kuwasaidia kujikimu.

SHARIFA: Hii ni mara ya pili unataja shimo! Tunapenda wafanyakazi wanaofanya kazi bila kutusumbua kwa haya na yale. Shimo! Shimo! Shimo!

NAMBI: Siwasumbui. Naomba tu mnilipe mshahara wa miezi mitano niliyofanya kazi (uk. 36).

Hali iliyomkabili Nambi ya kutolipwa mshahara kwa muda wa miezi mitano tangu aanze kazi ni jambo la kawaida miongoni mwa waajiri katika mataifa ya Mashariki ya Kati kama anavyosema Dudley (2009) kuwa hilo ni tatizo kubwa sana huko. Anasema kuwa wanawake hulipwa mishahara duni zaidi ikilinganishwa na kazi wanazofanya au hata kutolipwa kabisa hadi wakati mkataba unapoisha. Bales (2016) anadai kuwa mishahara ya wafanyakazi wa nyumbani huzuiliwa kama njia ya kuwadhhibiti ili wahakikishe wanawategemea waajiri wao na kuwatii. Bales anasema huu si tu unyonyaji wa kiuchumi bali ni ukiukaji pia wa haki za binadamu unaoendelezwa na uhitaji wa kilimwengu wa huduma kwa malipo duni.

3.2.4 Dhuluma za Kingono

Dhuluma za kimapenzi pia zinaakisiwa katika tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia*. Anwar, bwana mwenye nyumba, anaanza kumtongoza Nambi (kur. 52-57). Anamwambia kuwa kazi za nyumba zina sura mbili, za kuchosha na kuisisimua. Anaanza kumsogelea huku Nambi akisogea pia ili kuongeza umbali baina yao. Anamwahidi kuwa iwapo atakubali mambo yake, atapewa mshahara wake. Wakati hayo yakiendelea, Sharifa anabisha hodi. Nambi anapomfungulia mlango, anashuku kuna jambo walilokuwa wanaendeleza. Anamshambulia Nambi kwa kuyavuta masikio yake kwa nguvu, anampiga kofi. Anaenda jikoni kuchukua mwiko na kujaribu kumgonga nao begani lakini Nambi anakwepa. Baadaye, Nambi anampigia rafiki yake Halima simu kumsimulia changamoto anazopitia katika nyumba ya waajiri wake kama inavyodhihirika katika mazungumzo yafuatayo kupitia kwa njia ya simu:

NAMBI: Mara nyingi, najiona napigwa tu kama kifaa cha kufanyia mazoezi ya wanandondi.

HALIMA: Sikia ushauri wangu. Usijitupe kaburini. Tuliko kuuawa wafanyakazi ni jambo la kawaida. Mara kwa kisu, mara kwa kutupwa kutoka roshani. Kama wanaua watu hata bila chembe ya makosa, na je, ukiwapa udhuru? Naamini kwamba utafaulu kuepukana na idhilali inayokupata nyumbani mwa mwajiri, lakini usiwape udhuru kwamba ulitishia maisha yao.

NAMBI: Madhila ya kila siku yameniletea kuchanganyikiwa na akili mara kwa mara. Naona hata nimesahau kukushukuru kwa usaidizi mkubwa ulionipa (uk. 67).

Maneno ya Nambi kuwa, 'mara nyingi, naona napigwa tu kama kifaa cha kufanyia mazoezi ya wanandondi' (uk. 67) yanachora taswira ya mateso anayopitia. Halima anamshauri kuwa, huko waliko kuuawa kwa wafanyakazi ni jambo la kawaida kwa hiyo ajaribu kujizuia kadiri awezavyo kuwadhuru waajiri wake ili wasipate sababu ya kumtoa uhai. Hata hivyo, Sharifa anamuua Nambi anapomfumania na mumewe (kur. 76-77) wakati mume huyo akijaribu kumdhulumu Nambi kimapenzi.

Hali kama hiyo inawakabili wafanyakazi wengi wa nyumbani katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Waajiri wao wa kiume huanza kuwanyemelea na kutaka mapenzi ya kingono nao. Hata hivyo, visa hivi, kwa mujibu wa Jureidini (2010), huwa haviripotiwi. Anaendelea kusema kuwa dhuluma za kingono ni mojawapo ya aina ya unyonyaji unaowakabili wafanyakazi wa kike katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Kuna mchanganyiko wa mambo mengi ambayo hufanya iwe rahisi kwao kupitia dhuluma hizo. Baadhi ya mambo hayo ni ubaguzi wa rangi, kutegemea sana waajiri na kunyimwa uhuru wa kutangamana na wenzao. Tafiti nyingi zilizotangulia zinaonesha kuwa wafanyakazi hawa hudhulumiwa kimapenzi kwa kubakwa na

bwana mwenye nyumba pamoja na wanawe wa kiume kama wanavyosema Njiru na Laibon (2019).

Ripoti ya *Human Rights Watch* (2010) inaonesha kuwa wafanyakazi wengi waliripoti kuwa walikuwa wakipigwa, wakinyimwa chakula, wakifungiwa nyumbani na kufanya kazi kwa muda mrefu sana bila mapumziko. Bales (1999) anaona huu kama utumwa wa sasa usiomfunga mtumwa kwa mwajiri wake kisheria. Hata hivyo, mwajiri humtawala na kumdhibiti mfanyakazi wake kwa kutumia mashambulizi, vitisho na kukiuka haki zake kama binadamu.

3.2.5 Vifo

Kilele cha tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* ni kifo. Kama anwani ya tamthilia inavyoashiria, Nambi alitoka Afrika akiwa mzima, akarudi akiwa katika jeneza. Mara nyingi kifo ndicho huwa hatima ya wanawake wengi wanaokwenda kufanya kazi katika mataifa ya Mashariki ya Kati. Abder-Rahman, Al-Soleiti, Habash, AlAbdallat na Al-Abdallat (2021) walichunguza sababu za vifo hivi na kubaini kuwa vingi hutokana na kuanguka kutoka ghorofani, kujiua kutokana na mateso ya waajiri pamoja na msongo wa mawazo, mazingira duni ya kazi na mashambulizi ya kila aina yakiwamo kupigwa, kutukanwa na kubakwa. Hali hizi zinajitokeza kwenye tamthilia katika maisha ya Nambi. Nambi anatukanwa kila siku na Sharifa anayemtendea ukatili na kumuona kama mnyama wala si binadamu. Kwa upande ule mwingine, Anwar, mumewe Sharifa, anajaribu kumlazimisha katika tendo la ndoa kila wakati hadi mkewe anapomfumania akiwa anang'ang'ana kumvua nguo. Sharifa, kwa hasira, anamdunga Nambi kisu na kumuua. Hatimaye, Anwar anaita wasaidizi wampeleke hospitali huku akidai kuwa amejidunga kisu mara mbili akijaribu kujitua uhai kama inavyodhihirika katika mazungumzo yake ya simu:

ANWAR: [kwenye simu] Halo! Machela tafadhali! Nahitaji machela. Nyumba 664, Barabara ya Saeed Abu Abdullah.

[Anasikiliza] Mfanyikazi amejidunga kwa kisu mara mbili
[Anasikiliza] Ndiyo, ndiyo: jaribio la kujitua uhai. [Mlango unabishwa. Sharifa anaufungua bado akishikilia kisu. Wisam anaingia. Anapomwona Nambi sakafuni nguo zina damu anaangua kilio] (uk. 78).

Wisam anamuuliza mama yake kwa nini amemdunga Nambi kisu lakini Sharifa anasisitiza kuwa amejidunga mwenyewe, kauli ambayo Anwar anasisitiza kwa kusema kuwa alitaka kujiua (uk. 78). Kwa mujibu wa Abder-Rahman na wenzake (2021), vifo vingi vinavyoripotiwa hufanywa vionekane wafanyakazi walijiua wenyewe ingawa ni uongo tu. Mara nyingi wafanyakazi huuawa kwa kutiliwa sumu kwenye chakula, kupigwa na vifaa butu au kusukumwa kutoka ghorofani. Waajiri hujitetea kuwa walikuwa na msongo wa mawazo uliowasababisha kujitua uhai.

3.3 Hitimisho

Tamthilia ya *Jeneza Kutoka Saurabia* inaakisi sura mpya ya utumwa wa mwanawake katika karne ya 21. Wafanyakazi wa kike wanaokwenda kufanya kazi katika mataifa ya Mashariki ya Kati hupitia mambo magumu. Huenda huko kupitia kwa mawakala ambao huwapitishia kwenye mchakato unaogubikwa na udanganyifu. Mara nyingi mawakala hao hutumia udanganyifu na kutoa taarifa za uongo kuhusu ajira hizo ili ziwavutie waajiriwa. Ukiukaji wa haki za msingi za binadamu hudhihirika katika tafiti zilizofanywa na mashirika yasiyo kiserikali kuhusu suala hilo pia wakati ambao vyombo vya habari vinapotangaza kila mara kifo kinapotokea kutokana na dhuluma hizo. Wanawake hao pia huenda kwenye mitandao ya kijamii kueleza matatizo wanayoyapitia na hivi karibuni mwandishi wa tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia* ameliangazia suala hili katika tamthilia hiyo. Licha ya kuwa mashirika mengi yasiyo ya kiserikali yametafiti masuala haya na kupendekeza sheria ziwekwe kulinda haki za wafanyakazi wa nyumbani katika mataifa haya, bado mengi hayajafanywa. Aidha, wanawake wengi wanaendelea kwenda kufanya kazi katika mataifa hayo licha ya hatari ambazo huwakabili. Hali hii, kulingana na Idowu na wenzake (2021), inasababishwa na ufisadi, umaskini na ukosefu wa kazi katika nchi wanazotoka wanawake hao. Utafiti huu umechangia katika kuhakiki tamthilia ya *Jeneza kutoka Saurabia* na kuweka dhahiri changamoto wanazopitia wafanyakazi wa kike katika mataifa ya Mashariki ya Kati na Eneo la Ghuba. Mwandishi alitumia fasihi kama jukwaa la kuangazia suala hilo.

Marejeleo

- Abder-Rahman, H.A., Al-Soleiti, M., Habash, I.H., Al-Abdallat, I.M., na AlAbdallat, L.I. (2021). "Patterns of death among migrant domestic workers in Jordan: retrospective analysis of 63 cases in a tertiary hospital." *Katika Egyptian journal of forensic sciences*. 11(1) 24.
- Bales, K. (2016). *Blood and Earth: Modern Slavery, Ecocide, and the Secret to Saving the World*. New York: Random House.
- Bales, K. na Cornell, B. (2008). *Slavery Today*. Berkeley, California: Ground-Work Books.
- Bales, K. (2005). *Understanding Global Slavery: A Reader*. Berkley, California: University of California Press.
- Bales, K. (2002). "The Social Psychology of Modern Slavery." *Scientific American*. 286 (4) 80.
- Bales, K. (2012). "Disposable People: New Slavery in the Global Economy." California, Berkley: University of California Press
- Boyle, G. na Shields, L. (2018). "Modern Slavery and Women's Economic Empowerment." *DFID Work and Opportunities Programme*. <https://assets.publishing.service.gov.uk/media//modernslavery-womens-economic-empowerment.pdf>

- Campbell, G. (2004). *Structure of Slavery in Indian Ocean Africa and Asia*. London: Routledge.
- Daghar, M. (2020). *The new slavery: Kenyan workers in the Middle East* (ENACT Policy Brief No. 16). Enhancing Africa's Response to Transnational Organised Crime (ENACT). <https://respect.international/the-new-slaverykenyan-workers-in-the-middle-east>,
- D.B. (1985). *Slavery and Human Progress*. New York: Oxford University Press.
- Drescher, S. (2009). *Abolition: a history of slavery and antislavery*. New York: Cambridge University Press.
- Dudley, S. (2009) "Human Trafficking in the Middle East and North Africa Region," Human Rights & Human Welfare. <https://digitalcommons.du.edu/hrhw/vol9/iss1/31>
- IGG-GEO. (2020). *Women and modern slavery: An everyday, hidden reality*. <https://igg-geo.org/en/2020/05/24/women-and-modern-slavery-aneveryday-hidden-reality/>
- Human Rights Watch. (2010). *Walls at every turn: Exploitation of migrant domestic workers through the kafala (sponsorship) system*. Human Rights Watch. <https://www.hrw.org>
- Idowu, B. M., Arua, M. C., Nwosu, C. P., na Nwankwo, F. M. (2021). "Slavery in the Contemporary World: An Examination of Modern Slavery in Africa." *International Journal for Innovation Education and Research*, 9(8), 181-190. <https://doi.org/10.31686/ijer.vol9.iss8.3274>
- Ikuathu, S.N. (2017). Maudhui ya Ukoloni, Mamboleo katika Tamthilia Teule za Kiswahili. Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuucha Nairobi. (Haijachapishwa).
- Jureidini, R. (2010). "Trafficking and contract migrant workers in the Middle East." *Katika International Migration*, 48(4), 142-163. <https://doi.org/10.1111/j.1468-2435.2010.00609.x>
- Longhorn Publishers. (2019). *Kamusi ya Karne ya 21: Toleo la 4*. Nairobi: Longhorn Publishers.
- Lovejoy, P. E. (2011). *Transformations in slavery: a history of slavery in Africa* (Vol. 117). Cambridge: Cambridge University Press.
- Mann, M. (2010) "The Materialization of Human Trafficking in the Middle East and Impediments to Its Eradication," Human Rights & Human Welfare: Vol. 10: Iss. 1, Article 24. Inapatikana: <https://digitalcommons.du.edu/hrhw/vol10/iss1/24>
- Manzo, K. (2005). "Modern slavery, Global capitalism & Deproletarianisation in West Africa. Review of African Political Economy." No. 106:521-534. ROAPE Publications Ltd. Inapatikana <https://doi.org/10.1080/03056240500467013>
- Morgan, J. (2004). *Laboring women: Reproduction and gender in new world slavery*. Philadelphia, P.A.: University of Pennsylvania Press.

- Mutembei, A. K. (2016). "Slavery and Its Space in Kiswahili Literature." Katika *Asian Journal of African Studies*, (39), 3-31.
- Mutua, M. (2001). "Savages, victims, and saviors: The metaphor of human rights." Katika *Harvard International Law Journal*, 42, 201.
- Njiru, S. na Laiboni, N. (2019). Women's Labour Migration on the Africa-Middle East Corridor: Experiences of Migrant Domestic Workers from Kenya. Utafiti uliofadhiliwa na *Swiss Agency for Development and Cooperation*.
- Rami, F., Searight, H. R., Dryjanska, L., na Hall, M. C. (2025). Modern slavery and the United Nations Sustainable Development Goals. Katika *Canadian Psychology/Psychologie canadienne*. 66(4), 325-339. <https://doi.org/10.1037/cap0000429>
- Shureteh, H. A., Al-Khalili, R. K., na Neimneh, S. S. (2022). Sudanese Women, Slavery, and Race in Samiha Khrais's Novel *Slaves' Peanuts*. Katika *Interventions*, 24(6), 949-969.
- Sinha, M. (2021). "Treatment of migrant workers in the Middle East: Modern-day slavery?" Katika *ANU Undergraduate Research Journal*, 11(1), 144-154.
- Walk Free. (2023). *The Global Slavery Index 2023*. <https://cdn.walkfree.org/content/uploads/2023/05/17114737/Global-Slavery-Index-2023.pdf>
- Wa Mberia, K. (2025). *Jeneza Kutoka Saurabia*. Nairobi: Marimba Publications Ltd.